TCC

Tanzania Cigarette Public Limited Company
Rasilimali ya Tanzania



# Notisi ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TCC Plc

**Taarifa inatolewa kuwa, Mkutano Mkuu wa 61 wa wanahisa wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc) kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2025, utafanyika Hyatt Regency Kilimanjaro Hotel, Dar es Salaam Tanzania siku ya Ijumaa Mei 15, 2026, kuanzia saa 4:00 asubuhi.**

**Ajenda:**

1. Notisi na akidi.
2. Kuidhinisha Ajenda.
3. Kuthibitisha mhutasari wa Mkutano Mkuu wa 60 uliofanyika Aprili 23, 2025.
4. Yatokanayo na mhutasari wa kikao kilichopita.
5. Kupokea na kuthibitisha Ripoti ya Wakurugenzi na taarifa ya mahesabu ya mwaka iliyokaguliwa kwa mwaka unaoishia Disemba 31, 2025.
   - 5.1 Ripoti ya Wakurugenzi
   - 5.2 Taarifa ya mahesabu ya mwaka iliyokaguliwa kwa mwaka unaoishia Disemba 31, 2025
6. Kuidhinisha gawio.
7. Kuthibitisha wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka 2026.
8. Uteuzi wa Mkurugenzi wa Bodi.
9. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la malipo ya Wakurugenzi Wasiokuwa Watendaji.
10. Mengineyo

**Muhimu:**

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria mkutano atalazimika kuja na nakala ya risiti yake ya amana au cheti cha kushiriki pamoja na kitambulisho chake.
2. Mwanahisa mwenye haki ya kuhudhuria katika mkutano na kupiga kura anaweza kuteua mwakilishi ambaye atahudhuria katika mkutano na kupiga kura kulingana na katiba ya Kampuni.
3. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe katika ofisi za kampuni si zaidi ya Mei 13, 2026 saa 4 asubuhi.
4. Nakala za ripoti ya mwaka kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2025 zitatolewa kwenye ukumbi wa mkutano. Nakala tepe zitapatikana kwenye tovuti ya Kampuni.
5. Maelezo zaidi kuhusiana na mkutano huu yatapatikana kwenye tovuti ya TCC Plc (tcc.tz).
   Taarifa zaidi zitatumwa kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu na kwa barua pepe kwa wanahisa wanaostahili

**Kwa Idhini ya Bodi**

**Godson M. T. Killiza**
**Katibu wa Kampuni.**

RASILIMALI YA TANZANIA
65 Years